**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA**

**MAKONGORO HIGH SCHOOL**
**P.O. BOX 492,**
**BUNDA-MARA.**

**Mkuu wa Shule 0626 889 781**
**Makamu Mkuu wa Shule 0743893144**
**Mwalimu wa Nidhamu 0753360671**

KUMB.NA.MAKSS/STF/F.5/J.I/2026 08 APRILI, 2026

Mzazi/Mlezi wa MWANAFUNZI____________________________________

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAKONGORO KIDATO CHA TANO ILIYOPO HALMASHAURI YA BUNDA MKOANI MARA</u>**

**1.0** Ninafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha **TANO** katika shule hii Julai,2026.Hongera sana.Shule ya Sekondari Makongoro ina tahasusi za **PCM,PCB,EGM NA EBuAc** kwa kidato cha Tano na Sita.

Shule ya Sekondari Makongoro ni ya bweni kwa kidato cha **Tano** na **Sita**. Iko umbali wa ***Km 2½*** Mashariki mwa mji mdogo wa Nyamuswa, kandokando ya barabara kuu iendayo Mugumu Serengeti.Shule hii iko umbali wa ***Km 27*** kutoka stendi kuu ya mabasi ya wilaya ya Bunda. Mkoa wa Mara.Ufikapo Bunda stendi kuu ya mabasi panda magari yanayokwenda Mugumu wilaya ya Serengeti kupitia Nyamuswa,ukifika Nyamuswa mweleze kondakta akushushe kwenye geti la shule ya sekondari Makongoro.

Kwa wanaotokea Arusha wanaweza wakashuka shuleni au stendi ya nyamswa na kuchukua pikipiki kwa gharama ya shilingi elfu moja tu(1000) hadi shuleni.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **……………. Unatakiwa kuripoti shuleni siku moja kabla ya tarehe ya kufungua shule itakayotangazwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI.** Ofisi ya Makamu Mkuu wa shule itakuwa wazi kwa mapokezi na usajili ukiwa na:

i. "Pay in Slip" moja inayoonesha malipo uliyolipia
Benki Vifaa ulivyoandikiwa katika fomu hii,na fomu nne zilizo ambatanishwa na kujazwa kwa usahihi ***(fomu iliyojazwa na daktari, fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi, ahadi ya***

***mzazi, fomu ya kukubali masharti ya shule na fomu ya picha za wazazi na ndugu wa karibu*** *wa* mwanafunzi.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

## 2.1 SARE YA SHULE:

**(a) *Kwa Wavulana*:**

Ni suruali 02 nyeusi zenye marinda mawili na mifuko mitatu, pindo la chini (turn up); miwili pembeni na mmoja nyuma. Suruali isiwe modo na upana wa suruali usipungue inchi 16. Mkanda wa ngozi rangi nyeusi wa kuvalia suruali. Tai nyeusi, urefu usivuke mkanda wa suruali, upana sm 7½ na iwe na kibanio.

**(b) *Kwa Wasichana:***

Ni sketi 02 nyeusi zenye marinda, mkanda wa sketi (belti ya kiuno) usizidi inchi 1½ au sm 4. **Sketi ziwe ndefu zinazogusa kiatu.**
Tai nyeusi,urefu usivuke belti ya kiuno ya sketi,upana sm 7½ na iwe na kibanio.

***NB: Kumbuka kushona kitambaa kizito cha suti na sio kitambaa cha sukari sukari, ukija na sketi isiyogusa kiatu na suruali modo utarudishwa nyumbani mara moja kubadili hiyo sketi/suruali kabla ya kusajiliwa.***

**Kwa wasichana na Wavulana:**

- Shati 02 nyeupe zenye mikono mirefu.
- Soksi ndefu nyeupe jozi 02, zisiwe na urembo kwa wasichana.
- Soksi ndefu nyeusi jozi 02, zisiwe na urembo kwa wavulana.
- Viatu vyeusi vya kamba vyenye kufunika miguu viwe na kisigino kifupi na visipige kelele wakati wa kutembea kwenye sakafu.
- Sweta rangi ya bluu (Bluu halisi) aina ‘V ’shingo ya kuvaa wakati wa baridi.

(c) Kwa waislam wanatakiwa kuwa na hijabu rangi mbili (2) Rangi nyeupe na rangi ya bluu.

(d) **Sare za kushindia Jumatatu hadi Ijumaa kwa Wasichana.**
Ni sketi 02 za kaki mshono na kitambaa sawa na sketi nyeusi ( aje nazo).

(e) **Sare za jumamosi na jumapili**:

- ***Kwa wavulana;*** Suruali 02 za kaki zenye upana usiopungua inchi 16 na (aje nazo.).
- ***Kwa wasichana;*** Gauni 02 mshono wa solo kitambaa cha kunguru ya bluu kwa urefu wa kugusa viatu (aje nazo.)

**(f)Sare ya Michezo**:

- ***uKwa wavulana*** ni 'Track suit' ya rangi ya bluu (Bluu halisi),koti la track suit lisiwe na kofia, jezi ya rangi ya bluu na kaptra ya rangi ya bluu (isiwe na maandishi yoyote) na viatu vya raba nyeupe.

***Kwa wasichana*** ni 'Track suit' ya rangi ya bluu (Bluu halisi),koti la track suit lisiwe na kofia, jezi ya kijani na kaptura ya kijani (isiwe na maandishi yoyote ) na viatu vya raba nyeupe.

(g) **Sare ya kazi**:

- T-shirt' 02 zina collar (Tunashauri kila Mwanafunzi aje na Tsh.13,000/= kwa kila t-shirt Moja,ataelekezwa mahala pa kununua hizo t-shirt zenye nembo ya shule.Hii ni kutokana na sababu kwamba tunapoagiza kila mwanafunzi aje na t-shirt yake zinatofautiana rangi inayotakiwa pamoja na ubora unaotakiwa hivyo kupoteza ile dhana halisi ya sare za shule kwa kuwa kila mmoja atakuwa na sare yake inayotofautiana na ya mwanafunzi mwingine).

**NB: Mwanafunzi wa shule hii hapaswi kuja na nguo nyingine yoyote, tofauti na hizo zilizoelekezwa. Nguo za nyumbani hazitakiwi kabisa pamoja na vitu vya urembo pamoja na aina yoyote ile ya manukato.**

## 2.2 MICHANGO MBALIMBALI:

| Na | Aina ya michango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

Fedha yote ya michango ilipwe kwenye akaunti **Na.30101200050** Benki ya **NMB** na Jina la akaunti ni **RECURENT MAKONGORO SECONDARY. PESA TASLIMU HAZITAPOKELEWA**

**BIMA YA AFYA**

Mwanafunzi mwenye bima ya afya ya NHIF anatakiwa kuja nayo kwa ajili ya matibabu akiwa shuleni. Kwa mwanafunzi ambaye hana bima

ya afya Mzazi/Mlezi ni lazima kuchangia kiasi cha shilingi Elfu hamsini na mianne (50,400/=) kwa ajili ya kukatiwa bima ya afya ya NHIF atakayoitumia kwa ajili ya matibabu yake awapo shuleni. Pesa hii inalipiwa ofisini, tafadhali isiwekwe benki.

**2.3 Vifaa vya kazi:** .

- **a** Ufagio wa chelewa Mmoja (01) kwa ajili ya usafi wa nje kwa **PCM, PCB.**
  Soft bloom moja ( 01) kwa ajili ya usafi wa ndani kwa **EGM,EBuAc.**
- **b** Jembe moja na mpini wake kwa ajili ya usafi kwa **PCM,PCB,**
- **c** Ndoo ndogo mbili (02) za lita kumi zenye mifuniko kwa PCM, PCB,**EGM,EBuAc.**
- **d** Dawa ya chooni aina ya **DEXI** lita tano (5) kwa wanafunzi wa tahasusi ya **PCM,PCB,**
- **e** Hard bloom kwa ajili ya kusugulia sakafu **EGM,EBuAc.**
- **f** Squizer rubber (Mopa) kwa **PCM,PCB**
- **g** Shoka moja (1) na mpini wake lililonolewa kwa wanafunzi wa tahasusi ya **EBuAc** tu.

**2.4 Vifaa vya kutumia darasani na wakati wa mitihani**

- **h** Rimu (A4) ya karatasi Mbili (02) "**Double A" ZENYE COVER LA BLUU (kwa mwaka).**
- **i** Rulled paper Mbili (02) kwa muhula.
- **j** 'Counter Book' zisizopungua 11
- **k** 'Mathematical Set' 01
- **l** Rula ndefu 01 (30cm).
- **m** Kalamu blue au nyeusi za kutosha
- **n** 'Scientific Calculator' 01 (kwa tahasusi za **(EBuAc ,EGM,PCB,PCM).**
- **o** Vitabu vya masomo kulingana na tahasusi yake.
- **p** File Folder Moja (01) kwa ajili ya kutunzia taarifa zake.

**2.5 Vifaa binafsi vya kutumia bwenini:**

a) Godoro moja la 'sponge' '2½' x 6'
b) Chandarua (**NI LAZIMA**)
c) Garoni 01 ya Lita tano (05) kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa.
d) Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli kikombe na Kijiko **VIWE VYA**
e) **MFUPA NA SIYO PLASTIKI)**
f) 'Toilet paper' za kutosha (kwa matumizi yake binafsi)
g) Shuka 02 mpya *(rangi ya bluu)*
h) **Ndala/kanda mbili** za kuogea.
i) Taulo/khanga doti moja kwa wasichana
j) Blanketi 01 kwa ajili ya baridi.

k) Mto na foronya *(rangi ya bluu)*
l) **Ni vizuri aje na sanduku la bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake.**
m) Solata kwa tahadhari kama umeme ukikatika (**NI LAZIMA**)

**MUHIMU**

- **Kwa wale wanafunzi wenye masomo ya sayansi wanatakiwa waje na:-**
  **Dissection kit** – Kwa ajili ya upasuaji wa wanyama wadogowadogo katika maabara (**PCB)**.

- **Gloves box moja lenye PC 100 kwa tahasusi ya PCB tu.**

- **Laboratory coat** – Kwa ajili ya kuvaa wakati wa mazoezi ya maabara kuzuia madhara ya kemikali kwas tahasusi ya **PCB na PCM tu.**

- **Mask (barakoa) box moja lenye PC 100 kwa tahasusi ya PCM tu.**

- **Thermometer moja (0°c-100°c Alcohol) kwa tahasusi ya PCM na PCB tu.**

- **Vitabu vya ziada angalau viwili Kwa kila somo ili kurejea baada ya vipindi vya darasani,Viwe vya mtaala mpya.**

## 3.0 <u>SHERIA, KANUNI NA TARATIBU MUHIMU ZA SHULE HII:</u>

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.Mambo hayo ni Pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (Preparation).
iv. iv.Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

vi. Kutunza usafi wa mwili, Mavazi na mazingira ya shule.

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote..

ix. Kutunza mali za shule. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

x. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa.Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule.(Msiba au Ugonjwa).**

**3:2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi

ii. .Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.

iii. Kugombana na kuhamasisha mgomo.

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

v. .Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika.wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule, ila katika shule hii huruhusiwi kabisa kusuka nywele kwa mtindo wowote ule.

vii. Kufuga ndevu.

viii. viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.

ix. Uvutaji wa sigara.

x. Uasherati,Mahusiano ya jinsi moja,Ubakaji,kuoa au kuolewa.

xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba.

xii. Kusababisha mimba.

xiii. Kushiriki matendo ya uharifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.

xv. Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

xvi. Kudharau Bendera ya Taifa.

xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu;

xviii . Uharibifu wa mali ya umma kwa Makusudi.

**5:0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Tumia nafasi hii muhimu ambayo Taifa limekupa upendeleo maalumu. Ufikapo shuleni jitahidi kusoma kwa bidii ili uiokoe familia yako pamoja na Taifa kwa ujumla.**

Nafasi uliyopewa ni mlango wa kuingia katika **JAHAZ**I linalokuelekeza kwenye **BANDAR**I ya mafanikio katika maisha.Inabidi uitumie nafasi hii kwa uangalifu ukiweka juhudi zako zote katika maelekezo utakayopewa hapa shuleni,iwe ndani ya darasa au nje.**NIDHAMU**, UTIIna **USHIKIRIANO** ni mambo muhimu yatakayo kuwezesha kufikia mafanikio haya.Unatazamiwa kutafuta **MAARIFA** kukuza **TAALUMA**,kutunza **MAZINGIRA** na kuwa **MTIIFU.**

Mwisho napenda kukutakia maandalizi mema ya kujiunga na Shule ya Sekondari Makongoro.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**EZEKIEL S. MARWA**
**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (Wizi kwa njia ya Mtandao).Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa**

**simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE,NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-**

- **Mkuu wa shule: 0626 889 781**
- **Makamu mkuu wa shule:0743893144**
- **Mwandamizi Taaluma:0753360671**
- **Mwandamizi Malezi: 0747310262**
- **Matron:0768477775**
- **Patron :0763796914**
  **SHULE YA SEKONDARI MAKONGORO**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. JINA KAMILI LA MWANAFUNZI: ____________________

2. TAREHE YA KUZALIWA: ______________________

3. KABILA : ________________________

4. DINI: ____________________________

5. SHULE ATOKAYO:_________________________

6. MWANAFUNZI ANATOKA MTAA WA/ KIJIJI CHA ____________________

7. KATA YA: _________________TARAFA YA: _______________

8. WILAYA YA: _________________MKOA WA: ___________________

9. WAZAZI WOTE WAPO HAI.MMOJA YU-HAI/YATIMA (FUTA ISIYOHUSIKA)

10. JINA KAMILI MZAZI/MLEZI: _____________________________________

11. KAZI YA MZAZI/MLEZI: __________ KAMA MLEZI TAJA UHUSIANO____________

12. ANUANI YA MZAZI/MLEZI:______________________SIMU: ________

(a) Nimekubali nafasi niliyopewa na kuwa nitafuata sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Sheria zote na kanuni za shule nimezisoma na kuzielewa.

(b) Nitahakikisha na ninaahidi kuhudhuria darasani siku zote za masomo.

(c) Nitahakikisha nasoma kwa bidii na maarifa. Sitashiriki katika vurugu za aina yoyote ile pindi nikiwa mwanafunzi hapa Makongoro Sekondari. naahidi nitadumisha nidhamu nzuri hapa shuleni.

(d) Sitakuwa tayari kudhalilisha shule yangu.

(e) Nitakubali kuchukuliwa hatua stahiki endapo nitakapoenda kinyume na sheria za shule.

**JINA LA MWANAFUNZI**________________________________

**TAREHE**_________________________

FOMU **YA AHADI YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

**JINA LA MZAZI/MLEZI**: ________________________________________________

(a) Nimesoma na kuyaelewa maelekezo na sheria za shule ya Sekondari Makongoro aliyopewa mwanangu na ninakubaliana nayo.

(b) Ninakubali nafasi aliyopewa mwanangu.

(c) Nitahakikisha kuwa mwanangu anapata mahitaji yake yote muhimu ya shule.

(d) Nitakuwa bega kwa bega na walimu katika kuhakikisha kuwa mwanangu anafuata sheria na kanuni zilizo shuleni. Nidhamu nzuri ya motto ndiyo mafanikio yake.

(e) Naahidi kuwa mwanangu hatashiriki mgomo, fujo na wala makosa ya jinai kama yeye mwenyewe alivyoahidi. Ikitokea akikiuka hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.

________________________ _______________________

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI** **TAREHE**

____________________________________

**NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI**

## REQUEST FOR MEDIAL EXAMINATION

**THE HEADMASTER,**
**MAKONGORO SECONDARY**
**SCHOOL, P.O.BOX 492, BUNDA.**

20 June, 2025

The Medical Officer,
………………………………………..

**RE: …………………………………………………….. (Full Name of Student)**

Please kindly examine the above, named as to his/her Physical and mental for enrolment as a student, the examination should include the following categories.

1. (a) Eye – sight (b) Hearing (c) Limbs (d) Speech (e) Venereal diseases (f) Leprosy (g) Epilepsy
2. Neurosis
3. Pregnancy
4. Other serious diseases

**PART B**

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a government Medical Officer)
I have examined the above named person and consider that he/she is physically FIT/UNFIT and mentally FIT/UNFIT or full time of schooling.

1. (a) Eye – sight ………………………………………………………….
2. (b) Hearing ……………………………………………………………...
3. (c) Limbs …………………………………
   (d) Speech …………………………………………………… .
   (e) Venereal diseases …………………………………………………………
   (f) Leprosy ………………………………………………………………… (g)
   (g) Epilepsy………………………………………………………………
4. Neurosis ………………………………………………………………………
5. Pregnancy ………………………………………………………………..
6. Other serious diseases…………………………………………………………...

Date: …………………………………………… Signature: ………………………

Station: …………………………………… Designation: ……………………………..

**FOMU YA WAZAZI NA NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI WANAOWEZA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI PAMOJA NA TAARIFA ZAO MUHIMU.**

**Weka picha ya ndugu/mzazi 1**

Jina la mzazi au ndugu ……………………………………..
Uhusiano na mwanafunzi……………………………………
Namba za simu: …………………………. Au ………………
Kazi …………………………………………
Mahali unapoishi : Mkoa wa ……………………………….…………..
Wilaya ya ………….…………
Kata ya ……………….…………….. Mtaa/kitongoji cha………………………………...

**Weka picha ya ndugu/mzazi 2**

Jina la mzazi au ndugu ……………….……
Uhusiano na mwanafunzi…………………………………….
Namba za simu: …………………………. Au
Kazi : ……………………………………
Mahali unapoishi : Mkoa wa ………….……………..
Wilaya ya ………………..…………….………
Kata ya ……………………….….………
Mtaa/kitongoji cha…………………….

**Weka picha ya ndugu/mzazi 3**

Jina la mzazi au ndugu ………………………………
Uhusiano na mwanafunzi…………………………….…
Namba za simu: …………………………. Au
Kazi : …………………………………………..……...
Mahali unapoishi : Mkoa wa ………………………
Wilaya ya …………………..………
Kata ya ………………….….…………
Mtaa/kitongoji cha………………………